# HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

## MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA PILI 2023/2024 ULIOFANYIKA TAREHE 08.02.2024 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

***Mahudhurio:***

***Wahe. Madiwani:***

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Gerald Samwal Ng'ong'a | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Ezra Masana Bugingo | Diwani |
| 3. | Mhe. Ernest Marwa Sama | Diwani |
| 4. | Mhe. Albet Machiwa | Diwani |
| 5. | Mhe. Dalmas Nyagwal | Diwani |
| 6. | Mhe. Charles Chacha Nyambaki | Diwani |
| 7. | Mhe. Zuberi Mohamed Kinanda | Diwani |
| 8. | Mhe. Geofrey Samwel Juma | Diwani |
| 9. | Mhe. Joseph Ogaja Mbega | Diwani |
| 10. | Mhe. Juma Gradus Thondoe | Diwani |
| 11. | Mhe. Adriano Johanes Nyawambo | Diwani |
| 12. | Mhe. Jumanne Ally Oketho | Diwani |
| 13. | Mhe. Angelus Mwita Wambura | Diwani |
| 14. | Mhe. Paulo Martine Amuko | Diwani |
| 15. | Mhe. Laurent Abich Adriano | Diwani |
| 16. | Mhe. Julitha Athony Maige | Diwani |
| 17. | Mhe. Vivian Kyage Nyamabwa | Diwani |
| 18. | Mhe. Sylvana Ndemera | Diwani |
| 19. | Mhe. Fideria Otonya Rangi | Diwani |
| 20. | Mhe. Roja Lazaro Akuku | Diwani |
| 21. | Mhe. Nelson Ores Simba | Diwani |
| 22. | Mhe. Andericus Okwach Sariro | Diwani |
| 23. | Mhe. Deo Alfred Magori | Diwani |
| 24. | Mhe. Justine Rugoye Nyoswede | Diwani |
| 25. | Mhe. Felister Awil Nyakwaka | Diwani |
| 26. | Mhe. Samson Kagutu | Diwani |
| 27. | Mhe. Shelta John Mang'era | Diwani |
| 28. | Mhe. William Nestory Marwa | Diwani |
| 29. | Mhe. Edina Charles Oloo | Diwani |
| 30. | Mhe. Zablon Segere Mwita | Diwani |
| 31. | Mhe. Opino Beya Nickson | Diwani |
| 32. | Mhe. Khalphan Abdul Bimbireh | Diwani |
| 33. | Mhe. Ayoi Musa Sonde | Diwani |
| 34. | Mhe. Hellen Ezekiel Magige | Diwani |

***Wasiohudhuria kwa taarifa:***

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Jaffari W. Chege | Mbunge |

***Mahudhurio:***

***Watendaji:***

| | |
|---|---|
| 1. Adv. Abdul O. Mtaka | Mkurugenzi Mtendaji–Katibu |
| 2. Bw. Mbujilo G.M | Afisa Utumishi (W) |
| 3. Bw. Cosmas Mwantisya | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 4. Bw. Jumanne C. Obogo | Kaimu Afisa Usafirishaji |
| 5. Bi. Florentina Kashura | Kny: Mganga Mkuu |
| 6. Bw. Patrick Mathias | Kaimu Mdhibiti Mkuu Ubora wa Shule |
| 7. Bw. Paul M. Amos | Kny: Katibu Tume ya Walimu (TSC) |
| 8. Bw. Kessy Omary Hamisi | Afisa Tarafa |
| 9. Bw. Josephate Nyamwanda | Afisa Tarafa |
| 10. Adv. Alex Ifunya | Kaimu Mwanasheria wa Halmashauri |
| 11. Bw. Jairo Omeme | Kaimu Afisa TEHAMA |
| 12. Bw. Bartholomew B. Matoke | Kaimu Afisa Manunuzi |
| 13. Eg. Ramadhani Mcharo | Mhandisi wa Ujenzi |
| 14. Bw. Iman R. Mgonja | Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 15. Bw. Pauline Mathias | Kaimu Afisa Elimu Awali na Msingi |
| 16. Bw. Claud Katura | Kny: Afisa Maliasili |
| 17. Bw. James C. Chitumbi | Afisa Kilimo Mifugo na Uvuvi |
| 18. Bw. Lameck Meshack | Kny: Afisa Ardhi na Maliasili |
| 19. Bw. Salim M. Agwanda | Kaimu Afisa Biashara na Uwekezaji |
| 20. Mtuli T. Jumanne | Mratibu wa TASAF |
| 21. Bw. Comedius Mwananzila | Afisa Tarafa |
| 22. Bw. Julius O. Simeon | Afisa Tarafa |
| 23. Bw. Lameck Kulwa | Kny: Afisa Mipango na Uratibu |
| 24. Bw. Folkward Mchami | Afisa Elimu Sekondaria (W) |
| 25. CPA Hadhil Y. Ngayunda | Mweka Hazina (W) |
| 26. Bw. Abdallah S. Mikui | Afisa Utamaduni |

***Wageni waalikwa:***

| | |
|---|---|
| 1. Eng. Emmanuel Bernado | Kny: Meneja TARURA |
| 2. Eng. James Kishinhi | Meneja RUWASA |
| 3. Bw. Baraka Julius Aseno | Meneja REA |
| 4. Bw. Budeba Kihanda | Kny: Meneja TANESCO |
| 5. Bw. Peter Steven | Kamanda PCCB |
| 6. Bw. Mustapha K. Orwa | Katibu CCM Rorya |
| 7. A/Insp David | OCD Shirati |
| 8. A/Insp. Masoud | OCD Rorya |
| 9. Bw. Juma Salim | DSO |
| 10. Bw. Woz Kibwana | Jeshi la Akiba |

| | |
|---|---|
| 11. Bw. Siri Makanaki | Kny: Katibu CCM |
| 12. Bw. Songoma PMS | RS Mara |

***Waandishi wa Habari***

| | |
|---|---|
| 1. Bw. Frankius Cleophace | RFA / STAR TV |
| 2. Bw. Yohana Gitano | Habari Rorya |

***Sekretarieti:***

| | |
|---|---|
| 1. Bw. Rahan M. Amosy | Mwandishi wa Vikao vya Halmashauri |
| 2. Bw. Marline M. Matara | Mwandishi wa Vikao vya Halmashauri |
| 3. Bi. Florah M. Breck | Katibu Mahsusi |
| 4. Bw. William Kibasso | Mratibu wa Vikao |
| 5. Bi. Devotha Masiaga | Msaidizi wa Ofisi |
| 6. Bw. Paul Maloda | Cashier |

***Agenda:***

1. Kufungua Mkutano.
2. Utambulisho wa wageni.
3. Kusoma na kuridhia agenda.
4. Maswali ya papo kwa papo kwa Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri na Mkurugenzi Mtendaji (W).
5. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Kwanza 2023/2024 uliofanyika tarehe 17.11.2023.
6. Taarifa ya utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Kwanza 2023/2024 uliofanyika tarehe 17.11. 2023..
7. Muhtasari wa taarifa za Kamati za Kudumu kwa Robo ya Pili 2023/2024.
8. Masuala ya Kiutumishi/Kinidhamu.
9. Kufunga Mkutano.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.01/02/2024: KUFUNGUA MKUTANO**

Mwenyekiti aliwasalimu wajumbe wote waliokuwa wamehudhuria kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani kwa kipindi cha Robo ya Pili 2023/2024 na kuwakaribisha kwenye bunge la Halmashauri ya Rorya. Aidha aliwaomba kujadili hoja kwa umakini kwa maslahi mapana ya Halmashauri. Kisha alitamka kufungua mkutano mnamo saa 5:58 Asubuhi.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.02/02/2024: UTAMBULISHO WA WAGENI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya alimkaribisha Mwenyekiti wa Halmashauri ili aweze kuwakaribisha na kuwatambulisha wageni mbalimbali waliohudhuria kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Pili kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha Mwenyekiti alitambua uwepo wa Walimu kutoka Kata ya Roche, Kamati ya Ulinzi na Usalama na RAS.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.03/02/2024: KUSOMA NA KURIDHIA AGENDA**

Jumla ya agenda Tisa (09) zilizokuwa zimepangwa zilisomwa na kupokelewa na wajumbe. Aidha, wajumbe walizidhibitisha agenda hizo ili ziweze kujadiliwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Pili 2023/2024.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.04/02/2024: MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MHE. MWENYEKITI WA HALMASHAURI NA MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

Wajumbe waliojiorodhesha mapema kwa mujibu wa Kanuni walipewa fursa ya kuuliza maswali ya papo kwa papo. Aidha, wajumbe hao walipewa majibu na ufafanuzi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) na Mwenyekiti wa Halmashauri na wote waliridhika.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.05/02/2024: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA KWANZA 2023/2024 ULIOFANYIKA TAREHE 17.11.2023.**

Muhtasari wa Mkutano wa Baraza la Madiwani Robo ya Kwanza 2023/2024 uliofanyika tarehe **17.11.2023,** ulisomwa na kupokelewa na wajumbe. Aidha, wajumbe waliupitia muhtasari huo, hatimaye waliuthibitisha ili kumbukumbu halali ya vikao vya Baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.06/11/2023: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ROBO YA KWANZA 2023/20234 ULIOFANYIKA TAREHE 17.11.2024**

***Kipengele kilichohusu dampo la Shirati***

***Azimio:***

Iliazimiwa kwamba kamati ya Maendeleo ya kata ya Mkoma watafute eneo la kuhamishia dampo kwa ajili ya usalama wa wakazi.

***Utekelezaji:***

Utekelezaji ulifanyika na eneo lilipatikana taarifa itawasilishwa.

***Azimio:***

Iwasilishwe taarifa ya utekelezaji wa eneo lililopatikana kwa ajili ya dampo katika mji wa shirati na utegi

***Kipengele kilichohusu Hoja za Ukaguzi***

***Azimio:***

Iliazimiwa kwamba kikao kijacho cha Mkutano wa Bazara la Madiwani iwasilishwe taarifa ya majibu ya Hoja za ukaguzi ambazo zilikuwa hazijajibiwa.

***Utekelezaji:***

Taarifa ya utekelezaji itawasilishwa pamoja na taarifa ya Ukaguzi Robo ya Kwanza 2023/2024 kwenye uwasilishaji wa taarifa za Kamati.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.07/02/2024: MUHTASARI WA TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU KWA ROBO YA PILI 2023/2024**

Wenyeviti wa Kamati za Kudumu (Kamati ya Elimu, Afya na Maji, Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira, Kamati ya Maadili, Kamati ya Kuthibiti UKIMWI na Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa kamati zao kwa kipindi cha Robo ya Pili 2023/2024 na taarifa hizo zilipokelewa na wajumbe na kisha kutoa ushauri na maelekezo kama ifuatavyo: -

**Kipengele kilichohusu Mapato na Matumizi**

- Wajumbe walipongeza ukusanyaji wa mapato umekuwa mzuri na mapato ya halmashauri yanapanda, aidha waliomba baada ya kukusanya mapato hayo basi mapato hayo yarudi kwa wakati katika jamii ili kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo.
- Wajumbe walishauri kuendelea kusimamia kwa ukaribu mapato ya minada na mwalo kwa kuangalia sana minada bubu inayofanyika katika maeneo yetu.
- Wajumbe walishauri TARURA kusaidia ukarabati wa barabara za kiuchumi hasa zinazoelekea kwenye maeneo ya ukusanyaji wa mapato ili kuongeza uchumi wa Halmashauri na jamii kwa ujumla.

Baada ya ushauri na maoni wajumbe waliagiza kama ifuatavyo: -

**Azimio:**

Iliazimiwa kuwa iwasilishwe taarifa ya tathmini ya makusanyo ya mapato kwa nusu mwaka ili kuweza kupima utekelezaji wa bajeti.

**Kipengele kilichohusu Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

- Wajumbe walishauri kuwekwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 skimu ya chereche ili iweze kuboreshwa na kutoa huduma kwa jamii pamoja na ujenzi au ukarabati wa majosho.

Baada ya ushauri na kutoonekana kwa taarifa za taasisi yani RUWASA, TARURA na TANESCO wajumbe waliagiza kama ifuatavyo: -

**Azimio:**

Iliazimiwa kuwa iwasilishwe Taasisi ziandae baraza lao ili kujadili utekelezaji wa shughuli zao kwa kipindi cha Robo ya pili 2023/2024 kutokana na kutokuwasilisha taarifa kwenye Mkutano wa Baraza.

**KUMB.MUHT.BRZ.NA.08/02/2024: MASUALA YA KIUTUMISHI/ KINIDHAMU.**

Akiwasilisha taarifa hiyo Afisa Utumishi na Utawala aliwaeleza wajumbe kuwa uchunguzi wa Kaimu Afisa Manunuzi Ndg. Dominian Mpombe umekamilika kama ilivyoagizwa na kubaini makosa ya Kikanuni na utaratibu wa manunuzi yalikiukwa, hivyo Mkurugenzi anawasilisha kwa kamati kwa ajili ya ushauri na maoni.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo wajumbe waliagiza na kuelekeza kuwa hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi ya Ndugu Dominiani Mpombe kwa kukiuka taratibu na kanuni za manunuzi.

**KUMB. MUHT.BRZ.NA.09/02/2024: KUFUNGA MKUTANO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote waliohudhuria kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani na kuwapongeza kwa mjadala mzuri. Aidha aliwaomba taasisi kusaidia utekelezaji wa shughuli z Halmashauri ili kuwasaidia wananchi. Pia alipongeza timu ya mapato na Mkurugenzi Mtendaji kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato na kusisitiza kuongeza jitihada ili kufika lengo na Zaidi. Mwisho aliomba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na RAS isaidie kupata majibu ya mradi wa K.K.K (Kupima, Kupanga na Kumilikisha) ili kukamilisha mradi, kurejesha fedha na kuinufaisha Halmashauri kwa ujumla. Hatimaye alitamka kufunga mkutano majira ya saa 10:11 Jioni huku akiwatakia wajumbe wote safari njema.

**Muhtasari huu umethibitishwa na kusainiwa tarehe** 24/05/2024

**Sahihi**...................................

**Jina** ABDUL .O. MTAKA

**KATIBU**

**Sahihi**...................................

**Jina** GERALD .S. NGONGA

**MWENYEKITI**